TANGAZO LA SERIKALI Na. 1021 La Tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 41(1) (d))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

Jina
T.S Na. 26 la 2024

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024, ambazo katika Kanuni Ndogo hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6, kwa-

(a) Kufuta kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka kanuni ndogo ifuatayo:

"(2) Kamati itakuwa na wajumbe watano ambao ni maafisa wa Mamlaka watakaoteuliwa na Bodi kama ifuatavyo:

(a) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti Uchumi ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria;
(c) afisa sheria mmoja kutoka Kitengo cha Huduma za Sheria;
(d) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti wa Usafiri wa Reli; na
(e) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Udhibiti wa Usafiri wa Barabara.";

(f) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2), kanuni ndogo zifuatazo:

"(3) Akidi katika kikao cha Kamati itakuwa

ni wajumbe watatu.

(4) Maamuzi ya Kamati yatakua ni ya wajumbe wengi waliohudhuria.

(5) Kutakuwa na Katibu wa Kamati ambaye atateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kutoka miongoni mwa watumishi wa Mamlaka.".

Marekebisho ya kanuni ya 8

**3**. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8(1) kwa kuingiza maneno "kwa maandishi" yaliyopo kati ya maneno "yake" na "kwa".

Dodoma, AHMED MOHAMED AME

19 Novemba, 2024 *Mwenyekiti wa Bodi*